



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA



(TFRA)



IJUE
TFRA

UTANGULIZI

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ni Mamlaka ya Serikali chini ya Wizara ya Kilimo iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mbolea Na. 9 ya Mwaka 2009 kwa lengo la kudhibiti uzalishaji, uingizaji, usafirishaji na usambazaji wa mbolea nchini ili kuongeza tija ya kilimo na usalama wa chakula.

DIRA

Kuwa mdhibiti kinara kikanda katika kulinda ubora wa mbolea na kuhakikisha uzalishaji endelevu wa kilimo.

DHIMA

Kukuza matumizi salama ya mbolea, yenye tija na rafiki kwa mazingira kupitia udhibiti madhubuti, uimarishaji wa uwezo, utafiti, ubunifu na ushirikiano wa wadau.

MAJUKUMU

1. Kusimamia na kudhibiti ubora wa mbolea nchini.
 - Kusajili mbolea
 - Kufanya ukaguzi wa ubora wa mbolea katika mnyororo wa thamani.
2. Kudhibiti Utengenezaji, Uingizaji na Biashara ya Mbolea nchini.
 - Kusajili, kutoa leseni, kutunza kumbukumbu za watengenezaji na wauzaji wa mbolea nchini.
 - Kutoa vibali vya Uingizaji na Usafirishaji wa mbolea nje ya nchi.
 - Kusimamia bei za mbolea nchini.
 - Kuunganisha wauzaji na wanunuzi wa mbolea nchini ili kuhakikisha kwamba mbolea ya kutosheleza inapatikana kwa wakati.
3. Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na taasisi zingine juu ya masuala yanayohusu sera za usimamizi na udhibiti na biashara ya mbolea.
4. Kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuelimisha Umma juu ya matumizi sahihi ya mbolea.
5. Kushirikiana na Asasi za ndani na nje ya Nchi zinazoshughulikia mbolea katika kuhakikisha mbolea inamfikia mkulima katika ubora unaokubalika kwa bei nafuu





USAJILI WA MBOLEA NA VISAIDIZI VYA MBOLEA

Kila mbolea au kisaidizi cha mbolea kitasajiliwa na TFRA kabla haijaanza kutumika nchini kwa mujibu wa kifungu na. 8 cha Sheria ya Mbolea.

Hatua za kufuata ili kusajili mbolea mpya:

- ✓ Mwombaji atatakiwa kujaza fomu namba 1 katika Mfumo wa mtandao wa Mbolea unaopatikana kupitia fis.tfra.go.tz
- ✓ Fomu itakayojazwa ziambatishwe (upload) na maelezo kuhusu matumizi sahihi na maelezo kuhusu usalama wa mbolea (Material safety data sheet), picha ya kifungashio (label), cheti cha uchambuzi (Certificate of analysis / specification) na Sampuli ya mbolea.

USAJILI WA MTAMBO WA KUTAKASA (STERILIZING PLANT) NA KIWANDA CHA KUTENGENEZA MBOLEA (MANUFACTURING PLANT)

- Kwa mujibu wa kifungu 8 na 18 cha sheria ya mbolea, mtambo wa kutakasa na kiwanda cha kuzalisha mbolea lazima kisajiliwe kabla ya kuanza uzalishaji wa mbolea.
- Mwombaji atatakiwa kujaza fomu namba 5 katika mfumo wa mtandao wa Mbolea unaopatikana kupitia fis.tfra.go.tz
Baada ya kujaza mwombaji atatakiwa kuambatanisha (upload) cheti / hati ya umiliki wa mtambo au kiwanda (Particular of plant ownership), cheti cha taaluma cha afisa msimamizi (Academic and professional credentials of technical officer).



[tfra_official](#)



[tfraofficiall](#)

USAJILI WA MAENEO YA BIASHARA YA MBOLEA (PREMISE REGISTRATION)


- Kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha sheria ya mbolea kimeweka zuio la kuzalisha, kuhifadhi, kusambaza na kuuza mbolea isipo kuwa eneo hilo limesajiliwa chini ya sheria ya mbolea.
- Mwombaji anapaswa kujaza fomu ya maombi inayopatikana kwenye mfumo wa mtandao wa mbolea kupitia fis.tfra.go.tz
- Mwombaji anayeweza kupata huduma hii ni yule ambaye tayari amesajiliwa na kupata leseni ya biashara ya mbolea.
- Baada ya kujaza mwombaji atatakiwa kuambatisha (upload) cheti /hati ya umiliki au mkataba wa kupangisha eneo (Particular of plant ownership).

UTOAJI WA LESENI KWA WAFANYABIASHARA WA MBOLEA

Kifungu cha 13 cha sheria ya mbolea kimeweka masharti kwa mtu yeyote anayetaka kufanya biashara ya mbolea au uendeshaji wa mtambo wa utakasaji au kiwanda cha mbolea lazima awe amepewa leseni na TFRA ya kufanya biashara hiyo.

Hatua za kufuata ili kujisajili na kupata leseni ya kuuza mbolea:

- ✓ Mwombaji anapaswa kujaza fomu namba 9 kupitia mfumo wa mtandao wa Mbolea unaopatikana kupitia fis.tfra.go.tz.
- ✓ Mwombaji atatakiwa kuambatisha (upload) nakala ya cheti cha usajili wa kampuni au jina la biashara (Certificate of incorporation or certificate of registration of name), nakala ya cheti utambulisho wa mlipa kodi (TIN) na Nakala ya Cheti cha taaluma ya Kilimo au mafunzo ya mbolea (Proof of Academic or Participation/attending TFRA fertilizer dealership training)



KIBALI CHA KURINGIZA NCHINI (IMPORTATION PERMIT) NA KUSAFIRISHA NJE YA NCHI MBOLEA NA VIS Aidizi VYA MBOLEA

Kifungu cha 25 cha sheria ya mbolea kimeweka masharti ya kupata kibali cha kuingiza nchini na kusafirisha nje ya nchi mbolea na visaidizi vya mbolea.

- Kibali cha kuingiza nchini mbolea (Importation of fertilizer and fertilizer supplements).

Uingizaji Wa Mbolea Nchini Unafanyika Kwa Njia Mbili

1. Njia ya kwanza ni uingizaji wa mbolea kwa mfumo huria. Katika mfumo huu, kila mtu anaruhusiwa kuingiza mbolea ilimradi amefuata sheria na taratibu za uingizaji wa mbolea.
2. Njia ya pili ni kwa kutumia mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja. Mfumo huu unasimamiwa na Kanuni za Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja (The Fertilizer (Bulk Procurement) Regulations, 2017)

HATUA ZA KUFUATA KUPATA KIBALI CHA KURINGIZA MBOLEA NA VIS Aidizi VYA MBOLEA NCHINI (IMPORTATION OF FERTILIZER AND FERTILIZER SUPPLEMENTS)

- ✓ Kujaza fomu namba 16 katika mfumo wa mtandao wa mbolea unaopatikana kupitia fis.tfra.go.tz
Mwombaji anayaweza kupata huduma hii ni yule ambaye tayari amesajiliwa nakupata leseni ya biashara ya mbolea.
- ✓ Baada ya kujaza mwombaji atatakiwa kuambatanisha (upload)
 - Hati ya malipo (Commercial Invoice)
 - Hati ya kusafirisha mzigo (Bill of lading)
 - Cheti cha uchambuzi wa maabara kutoka kwa mtengenezaji (Certificate of analysis or certificate of quality)
- ✓ Baada ya maombi kupokelewa na kuidhinishwa mwombaji atapatiwa hati ya madai (Control Number) kwa ajili ya kulipia tozo (import fee)
- ✓ Baada ya kulipia atapewa kibali cha kuingiza mbolea.



tfra_official



tfraofficiall

HATUA ZA KUFUATA KUPATA KIBALI CHA KUSAFIRISHA MBOLEA NA VISAIDIZI VYA MBOLEA NJE YA NCHI (EXPORTATION OF FERTILIZER AND FERTILIZER SUPPLEMENTS)

Kwa mujibu wa Kifungu cha 25 cha Sheria ya mbolea, mtu yoyote haruhusiwi kutoa mbolea iliyopo nchini kwenda nje ya nchini isipokuwa tu amepata kibali kutoka TFRA.

HATUA ZA KUFUATA

- ✓ Mwombaji ajaze fomu namba 19 katika mfumo wa mtandao wa Mbolea unaopatikana kupitia fis.tfra.go.tz.
- ✓ Baada ya maombi kupokelewa na kuidhinishwa mwombaji atapewa hati ya madai kwa ajili ya kulipia ada (export fee).
- ✓ Baada ya malipo mwombaji atapewa kibali cha kusafirisha mbolea nje ya nchi.

NB: Mwombaji anayeweza kupata huduma hii ni yule ambaye tayari amesajiliwa na kupata leseni ya biashara ya mbolea.

WASILIANA NASI KWA MAELEZO ZAIDI

Kilimo Street , Kilimo House |
Complex Building, Mandela Road
P.O.Box 46238, 15471 Dar Es Salaam
0800110154/53 | +255 22 2861939
info@tfra.go.tz | www.tfra.go.tz

  [tfra_official](#)  [tfraofficiall](#)

